

GRADE 4
KISWAHILI
END-TERM-2-2023

VIUNGO VYA KUTATHMINI			
Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
4 30 - 40	3 20 - 30	2 11 - 19	1 0 - 10

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kuna ndege wa aina nyingi duniani. Kuna wale ambao hufungwa na wale wanaoishi kichakani. Kuku ni ndege anayefungwa. Huishi kwenye kizimba. Wale wa kichakani ni kama Chiriku, ninga na korongo. Kuna ndege ambao hula nyama kama mwewe. Ndege wengi wanaweza kuburuka na kupaa ila mbuni ambaye ndiye ndege mkubwa kuliko wote. Ndege wa kichakani kama njiwa na mnana hujenga viota vyao mitini. Keremkeremu ni ndege wa ajabu. Yeye hupenda kula nyuki ilhali sisi binadamu hupenda kula asali ya nyuki.

- | | |
|---|---|
| <p>1. Makao ya kuku huitwa?</p> <p>A. Kizimba B. Kiota
C. Zizi D. tundu</p> <p>2. Ni ndege yupi haishi kichakani</p> <p>A. Chiriku B. Ninga
C. Korongo D. Kuku</p> <p>3. Ni ndege yupi hula nyama kulingana na taarifa.</p> <p>A. njiwa B. keremkeremu
C. mwewe D. mnana</p> | <p>4. Ni ndege yupi ambaye hawezi kupaa?</p> <p>A. chiriku
B. kuku
C. mnana
D. Mbuni</p> <p>5. Binadamu hula asali, keremkeremu hula:-</p> <p>A. nafaka
B. nyuki
C. samaki
D. nyama</p> |
|---|---|

Soma kifungu kifuatacho kisha jibu maswali 6 hadi 9

Mutiso alizaliwa mjini. Tangu kuzaliwa alikuwa hajaenda shambani. Yeye alikuwa hajaona mnyama yeyote wa msituni. Mnyama aliyemjua ni paka tu. Mutiso alikuwa na rafiki yake. Wao walikuwa wakisoma shule moja. Jina la rafiki yake lilikuwa Wafula. Wazazi wa wafula walikuwa wakiishi shambani. Siku moja Mutiso alifuatana na wafula kwenda shambani. Njiani mutiso aliona vitu na wanyama wengi.

Wazazi wa Wafula walimkaribisha Mutiso vizuri. Mutiso alipewa vyakula vya shambani. Alikunywa uji wa wimbi. Pia alikula ufuta na mahindi. Baada ya kula, Mutiso alitembeatembea.

- | | |
|--|---|
| <p>6. Mutiso alizaliwa wapi?
A. Shambani B. Kijijini
C. Nyumbani D. Mjini</p> <p>7. Ni kauli gani si ya kweli kulingana na aya ya kwanza ?
Mutiso alikuwa _____
A. hajaenda shambani
B. hajaona mnyama yeyote
C. hajaona mnyama wa msituni
D. rafiki ya Wafula.</p> | <p>8. Wazazi wa Wafula walikuwa wakiishi:-
A. Shambani
B. Mjini
C. Kijijini
D. hatujaambiwa</p> <p>9. Ni chakula gani ambacho hakikutajwa kati ya vile ambavyo Mutiso alipewa
A. Uji B. ufuta
C. Ugali D. mahindi</p> |
|--|---|

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 10 hadi 12.

Wanyamapori wana faida kubwa sana katika nchi yetu. Wanyama hawa huleta pesa nyingi nchini mwetu. Wageni kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni huja kuwaona wanyama huku kwetu. Wageni hutembelea mbuga za wanyama na kulipa pesa nyingi. Wageni hawa hujulikana kama watalii.

Nchi yetu ya Kenya imebarikiwa kuwa na wanyama kama vile simba, ndovu, duma, kifaru na wengineo. Wanyama hawa hawapatikani katika nchi nyingi za ulaya. Hii ndiyo maana wazungu huja kuwaonea huku kwetu.

- | | |
|--|---|
| <p>10. Ni kauli gani si kweli kuligana na aya ya kwanza?
A. Wanyama pori huleta hasara.
B. Wanyama pori huleta pesa nyingi.
C. Wageni huja kuwatazama wanyama pori.
D. Wageni hulipa pesa nyingi.</p> <p>11. Mtu anayetembelea mahali panapovutia kwa ajili ya kujifurahisha huitwaje?
A. Mzalendo</p> | <p>B. Mtalii
C. Mlowezi
D. Mkimbizi</p> <p>12. Nchi ya Kenya imebarikiwaje?
A. kuwa na wakimbiaji.
B. kuwa na wanyama.
C. kuwa na mali asili.
D. kuwa na watalii.</p> |
|--|---|

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 13 hadi 15.

Siku ya kufunga shule huwa na shunguli nyingi sana. Wale ambao husomea shule za mabweni huwa wametingwa na furaha zaidi. Sijui kama ni kwa sababu wataungana na familia zao au ni kwa sababu ya chakula. Siku hiyo wanafunzi huamka asubuhi na mapema baada ya kulala usingizi wa mangemungemu.

- | | |
|--|--|
| <p>13. Siku ya kufunga shule huwa
A. na shughuli nyingi
B. ya huzuni sana
C. na mateso mengi
D. Ya woga sana</p> <p>14. Ni akina nani huwa na furaha zaidi?
A. wasichana
B. Wavulana</p> | <p>C. Wanafunzi wa bweni
D. Wanafunzi wa kutwa.</p> <p>15. Usingizi wa mangemungemu ni usingizi
A. Mzito
B. Mwepesi
C. Mnono
D. Ambao mtu hajisikii.</p> |
|--|--|

Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 mpaka 20.

Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Usiku _____16_____ mama alitayarisha chakula _____17_____. Kilikuwa _____18_____ wa kuku na ugali. Baada ya kukiandaa mezani _____19_____ tulikusanyika _____20_____.

- | | | | |
|-----------------|-------------|-------------|--------------|
| 16. A. huo | B. huyo | C. hiyo | D. hilo |
| 17. A. tamu | B. mtamu | C. kitamu | D. mitamu |
| 18. A. michuzi | B. mchuzi | C. mchuuzi | D. michuuzi |
| 19. A. zote | B. yote | C. wote | D. sote |
| 20. A. uwanjani | B. darasani | C. sebuleni | D. vitandani |

Kutoka swali la 21 hadi 30, chagua jibu sahihi

21. Chagua kivumishi katika sentensi ifuatayo
Vipepeo wale walipuliziwa dawa.
A. Vipepeo
B. wale
C. walipuliziwa
D. dawa
22. Chagua kitenzi katika sentensi ifuatayo
Mama mnene analima shambani
A. Mama
B. mnene
C. analima
D. shambani
23. Jibu maamkizi yafuatayo.
Habari yako?
A. mzuri
B. zuri
C. jema
D. Njema
24. Tumia kiunganishi sahihi.
Alikuwa _____ sikumwona.
A. waia
B. na
C. lakini
D. kwani
25. Ni sentensi gani sahihi?
A. Rinda lipya limetengenezwa.
B. Nguo zipya zimeibwa.
C. Gari jipya ni hili.
D. Kalamu kipya kinapendeza.

26. Andika umoja wa sentensi zifuatazo.

- A. Viti vyake vimevunjika.
B. Kiti chao kimevunjika.
C. Viti vyake kimevunjika.
D. Kiti chake kimevunjika.
27. Neno "Mpira" liko katika ngeli gani?
A. U - ZI
B. U - I
C. U - U
D. I - ZI
28. Tumia o-ote kwa usahihi.
Nguo _____ itakufaa
A. zozote
B. yeyote
C. yoyote
D. lolote
29. Tegua kitendawili.
Popoo mbili zavuka mto
A. macho
B. miguu
C. popo
D. marafiki
30. Tumia kiulizi sahihi.
Ni wanafunzi _____ walienda katika ziara?
A. yupi
B. ngapi
C. gani
D. wagani

